# SOMO: MWENYE KUANGALIA UPEPO HATAPANDA

# MAANDIKO: MHUB 11:4-5, 2WAF 7: 1-2

1. **UTANGULIZI**

   Katika Ulimwengu huu, mazingira yanayotuzunguka yanakuwa na nafasi kubwa sana ya kutukatisha tamaa au kutujengea roho ya woga ambayo inafanya kazi kubwa sana ndani ya mteule ya kukata channels zote!! ( **channel ni njia ambayo mawimbi ya sauti yanarushwa angani ili yasikike katika radio, TV au simu);** Kwa hiyo mteule anapoishi kwa kuangalia mazingira yanayomzunguka , mawasiliano yake na Mungu aliye hai yanakatwa kabisa jambo ambalo linamfanya akate tamaa na hivyo kujaa roho ya woga ndani yake ambayo kwa vyovyote itamletea madhara baadae. **Kuogopa jambo kwa sababu ya mazingira yanayoonekana sasa/leo mbele yetu, ni ishara ya kupoteza kabisa baraka pamoja na mambo mazuri yaliyo mbele yetu.**

- Siku ambayo mteule amepambana na mazingira yanayokatisha tamaa ambayo ni lazima kila mtu atakutana nayo katika maisha haya kwanza kabla ya kwenda kiwango kingine cha kiroho **siku hiyo inakuwa ndefu sana (ni kama haiendi), usiku unakuwa mrefu sana maana hupati usingizi, moyo unakwenda mbio (B.P) inapanda au inashuka; na unaweza kufadhaika na kukata tamaa na kuanza kulia mwenyewe na kujikatia tamaa ya kuishi kabisa. *Hesab. 13: 26-33,14:1-4* ama kwa hakika siku mtu anapambana na mazingira magumu anayoyaogopa inakuwa siku ndefu mno kuliko siku ya kazi ya kawaida.**

2. Mtume Petro ambaye alipitia mazingira kadhaa magumu sana ndiye aliyeandika kwa ufunuo juu ya jambo hili pale alipofananisha kipindi hiki cha mazingira magumu kwa mtu wa Mungu kama simba aungurumae akitafuta mtu ammeze ***1Petr 5:8***. Kipindi unakabiliana na mazingira magumu, ni kipindi ambacho mazingira yatatumia kila aina ya mbinu ili

**kukutisha** kwa lego kubwa moja kwamba ukate tamaa/uogope na kisha uiache imani ***!! Mdo 4:13-22, 5:17-21-29.***

- Petro alipata ufunuo dhahiri kwamba mazingira yanatumiwa na shetani ili kutisha wateule, na endapo wataangalia mazingira yanayowazunguka badala ya kuangalia ahadi za Mungu kwao pamoja na neno lake, hakika watamezwa. "**Yapo mazingira ukiyatazama kwa macho haya ya nyama – YANATISHA"** yanaogopesha hasa!!

***Mfn***.a.Kilichomfanya Yona aogope kwenda Ninawi baada ya Mungu kumtuma kwenda kuhubiri Injili huko ni historia aliyokuwa nayo ya ukatili wa Mfalme wa Ninawi ya kukata kila kichwa cha Manabii wa Mungu na kukikausha na kisha kuvitundika vichwa hivyo katika barabara kuu iliyokuwa inaingia Ninawi hadi Ikulu ya Nchi. Kwa mazingira ya namna hii, mtu anaogopa kwenda katika Nchi hii hata kama Mungu angesema naye!!! Kwa kitendo chake Yona cha kukimbia Mungu akamweka katika mazingira magumu zaidi siku tatu usiku na mchana na kisha akajikuta yuko Ninawi!!! Na alipotii na kuanza kuhubiri, nchi ya Ninawi na Mfalme wake wakawa na toba ambayo hadi leo haijawahi kufanywa na Taifa lolote duniani!!! ***Yona 1: 1 – 17, 2: 1 – 10, 3: 1 – 10.*** **Mazingira ya ibilisi yanatisha, lakini Mungu tuliye mwamini matendo yake yanatisha zaidi.**

b. Yule Akida wa Samaria alipoangalia mazingira ya watu walivyokuwa wanakula mavi ya njiwa na vichwa vya punda pamoja na kula watoto wao; halafu aambiwe na Nabii Elisha kwamba kesho unga mzuri utauzwa kwa bei nafuu katika lango la Samaria – aliona huo ni upuuzi, ni jambo lisilowezekana kamwe!! **mazingira yanakatisha tamaa; yanachosha, na endapo hatutaangalia Mungu anasemaje na ahadi zake kwetu zikoje hakuna atakayevuka salama katika kizingiti hiki cha mazingira**

**ambacho shetani anakitumia kama silaha yake kubwa ya kukatisha watu wa Mungu tamaa ya kumwamini Mungu na ahadi zake.**

3. Sikia watu wakubwa katika kikao hiki **wanachokiamua** "***Mdo. 4: 15- 18, 5: 24 – 28.*** Hii njia ya kuwatisha Mitume ndiyo njia iliyoonekana kuwa bora kuliko njia nyingine zote!! na kweli hata leo ukikutana na mazingira magumu baada ya kuokoka halafu ukasimama imara bado bila kutetereka; shetani atakuwa amekushindwa kabisa na Mbinguni utaingia!! Aliweka mazingira magumu sana ili Mtume Paulo aogope lakini akakwama- ***Mdo. 14: 19 – 22, 16: 19 – 25, 27: 21- 26*** n.k. sikia hata Nebkadreza anavyowakatisha watu wa Mungu **– Dan. 3:15***
   Daudi kijana hakuangalia upepo (Goliathi bali alimwagalia Mungu na akashinda.) ***1Samwl. 17: 31 – 55***

**Note: Kukumbuka daima ukuu wa Mungu katikati ya mazingira magumu unayokabiliana nayo ndiyo njia ya ushindi mkuu katika maisha yetu ya wokovu kama Daudi.** ***Zab. 29: 3-11, 1Samwl. 17:33-37***

Nabii Elisha hakuogopa kusema kila ambacho Mungu alimtuma aseme eti kwa sababu ya kuogopa mazingara na wana akafanya muujiza!! **Bwana alimkemea Abrahamu na mkewe Sara akawataka wasiangalie mazingira bali wamwangalie Bwana!!** ***Mwanz. 17: 15 – 19, 18: 8-15*** na kweli wakampata Isaka (kicheko) katika umri ambao dunia ilishasema basi

- Mazingara yamefikisha watu kutotaka kuolewa tena leo, kutotaka kuzaa tena (wanataka katoto kamoja tu au viwili mwisho!!) mazingira yamefanya watu wa Mungu kukwepa wito leo!! (mavuno ni mengi lakini watenda kazi hakuna!!! ***Math. 9: 37 – 38***- Hakuna anayetaka kwenda kufanya kazi vijijini hata ya kuajiriwa!!! Mazingira yamefanya hata wateule hawakaribishani tena majumbani mwao!!! Mazingira yamefanya wateule kuogopa siasa leo; kuogopa kumkiri Yesu hadharani!!

- Mfalme Suleimani anasema wazi kwamba mtu akiangalia upepo, hatapanda (yeyote anayengojea hali ya hewa iwe nzuri, fedha ziwe nyingi ndipo awe mtoaji kamwe fedha huwa haiwi nyingi kwa mtu isiyo na kazi, na anaenda mbali zaidi pale anaposema kwamba atazamaye mawingu hatavuna!! mazingira yataendelea kuwa magumu zaidi kadri Yesu anavyokaribia kurudi na kadri utakavyoendelea kuyaokodolewa macho. Ni wale tu ambao hawataangalia mazingira kwa macho haya ya nyama, bali watamwangalie Yesu na neno lake. Ndiyo watakaopata matokeo chanya.

**Onyo:Katika mazingira magumu tusijaribu *kamwe kuomba maombi ya kumtisha Mungu*- hatishiki!! *Kut. 32:30-35.***

***Note:* Katikati ya Mazingira magumu Esta hakupoteza heshima yake na akamwona Mungu akitenda jambo la ajabu – *Esta 2: 15 – 17;*** katikatika ya mazingira magumu sana ya kuuawa, Mordekai alimwona Mungu. ***Esta 5: 12 -14, 6: 1* – 12;** Katikati ya mazingira magumu Sara alimwona Bwana - **Mwanzo 21: 1 – 7,** nasi leo katikati ya mazingira magumu, hakika tutamwona Mungu. Tusiangalie upepo, tusiangalie mazingira; kama Mungu anafanya uumbaji tumboni kwa njia ambayo hakuna mtu ajuaye, hata katikati ya mazingira magumu yaliyopo sasa duniani, tutavuka tu kwa Jina la Yesu Kristo. ***Amina.***

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***July 2021***